**MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA HALMASHAURI KILICHOFANYIKA TAREHE 17-18/05/2017 KATIKA UKUMBI WA RUTESCO.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Rashidi Nakumbya | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Shabani Kambona | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Elias Nkane | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Rashidi Nnunduma | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Jafari Mwambe | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mikidadi Mbute | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Issa Ngongonda | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Awesa Napindu | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Paulina Mmuya | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Omari Pendeka | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Ansila Lukanga | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Abdala Nachingi | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Selemani Likuche | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Selemani Tulinje | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Amina Naenje | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Jafari Chande | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Hidaya Mtojima | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Bakari Mpanyangula | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Omari Liwikila | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Saidi Kawale | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Andrew Chikongwe | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Omari Songea | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Zainabu Nnunduma | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Shemsia Madebe | Mjumbe |
| 25. | Mhe. Zuwena Kitatichingi | Mjumbe |
| 26. | Mhe. Abdala Chigope | Mjumbe |
| 27. | Mhe. Mekitdis Wilbarti. | Mjumbe |
| 28. | Mhe. Kassian Chitanda | Mjumbe |
| 29. | Mhe. Juma Kambona | Mjumbe |
| 30. | Ndg. Eng Lawrence Mapunda | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji –Katibu |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Kassimu Majaliwa (MB) | Mjumbe kwa Taarifa. |
| 2. | Mhe. Daniel Mtawa | Mjumbe – kwa ugonjwa. |

**WATENDAJI WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Thomas Luambano | Mkuu wa idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 2. | Ndg. Yusuf Chilumba | K/Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 3. | Ndg. Benedict Kwesiga | K/ Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 4. | Dr. Japhet Simeo | Mkuu wa Idara ya Afya |
| 5. | Ndg. Grace Mwambe | Mkuu wa Idara ya M/ Jamii, Ustawi na Vijana |
| 6. | Ndg. Festo Mwangalika | Mkuu wa Idara ya Utumishi na utawala |
| 7. | Eng Mashaka Nalupi | Mkuu wa Idara ya Ujenzi na Zimamoto |
| 8. | Ndg. Zuhura Makota | K/Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Ndg. Bihuria shaabani | K/Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 10 | Ndg. Anthony Mandai | K/Katibu TSC |
| 11 | Eng. Joshua Kabange | K/Mkuu wa Idara ya Maji |
| 12 | Ndg. Eligy Gaundele | K/Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 13 | Ndg.Jumanne Kalalula | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani |
| 14 | Ndg. Frank Chonya | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 15 | Ndg.Henry Helahela | K/Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 16 | Ndg. Moses Mkwesela | K/Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 17 | Ndg .Oscar Magoge | K/Mkuu wa Kitengo cha Ugavi |
| 18 | Ndg. Mwanakheri Ally | Afisa Habari. |
| 19 | Ndg. Violeth Byanjweli | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Chakula na Ushirika |
| 20 | Ndg Sophia Hokororo | Mkuu wa idara ya uthibiti wa shule. |

**WAALIKWA WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. J. Mkirikiti | Mkuu wa Wilaya |
| 2. | Ndg . Prospar Roman | Afisa Serikali za Mitaa Lindi |
| 3. | Ndg. B. Esau | Katibu CCM (W) |
| 4. | Ndg. Kenedy Kisura | Mwandishi wa Habari Gazeti la Habari Leo |
| 5. | Ndg. S.Nang'endeku | KNY Mwenyekiti Chama cha CUF |
| 6. | Ndg. Mauridi Chitanda | Kny Mwenyekiti CHADEMA |
| 7. | Ndg. Jongo sudy | Mwandishi wa Habari Radio Ruangwa. |
| 8. | Ndg .C.Lilai | Mwandishi wa Habari Gazeti la Mwananchi |
| 9. | Ndg. S.Namanga | Afisa Tarafa Ruangwa. |
| 10. | Ndg. Msonga Matiku | Afisa Tarafa Mandawa. |
| 11. | Ndg .Tito Said | K/Afisa Tarafa Mnacho. |
| 12. | Ndg. Fabian Joseph | Mwandishi wa Habari Radio Ruangwa. |

**SEKRETARIETI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Bashiru Mkauchumbe | Mwandishi wa Mikutano. |

**AGENDA NA 1/5/2017 KUFUNGUA KIKAO.**

Kabla ya kufungua kikao uliimbwa wimbo wa Taifa pamoja na Dua ya kuliombea Baraza,baada ya matukio hayo Mh. Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 4.30 asubuhi.

**AGENDA NA.2/5/2017 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA KUTOKA KWENYE KATA**

Mh.Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kwamba kila Mh.diwani wa kata atawasilisha taarifa za utendaji kazi kwenye kata yake ya kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2016/2017.Katika taarifa hizo wajumbe walijikita zaidi katika kutoa changamoto zilizopo kwenye kata zao kama ifuatavyo:-

**1.KATA YA NARUNGOMBE**

Diwani wa kata ya Narungombe Mh.Elias Nkane aliwasilisha taarifa ya kata yake kwa kutoa changamoto za kata yake ambazo ni pamoja na:-kutokuwepo kwa barabara ya kudumu kati ya Liuguru – Narungombe,upungufu wa nyumba za walimu katika shule ya sekondari Narungombe na Liuguru pamoja na vyumba vya maabara, upungufu wa walimu katika shule za msingi na Sekondari katika kata hiyo,kutopewa fedha za ushuru wa mbaazi katika vijiji vya Narungombe na Liuguru.

**2.KATA YA MATAMBARALE**

Changamoto zilizowasilishwa katika kata hiyo na Mh.Kitatichingi kwa niaba ya Diwani wa kata hiyo ni pamoja na kijiji cha Matambarale kusini hakina Afisa Mtendaji wa kijiji na Afisa Maendeleo ya Jamii wa kata,upungufu wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu katika shule za msingi Nandandala na Namkatila ,Kata haina shule ya sekondari japo mipango tayari imeshawekwa ya kuanzisha ujenzi wa shule ya sekondari.

**3.KATA YA MANDAWA**

Mhe.Nachingi aliwasilisha taarifa ya kata yake ikiambatana na changamoto za kata hiyo, Kuendelea kwa kilimo cha kuhamahama japo elimu inaendelea kutolewa, changamoto wananchi kutohudhuria mikutano ya vijiji japokuwa kiasi fulani tatizo limeanza kupungua baada ya kutolewa elimu kwa wananchi,uharibifu wa mazingira,migogoro ya mipaka ya ardhi,kutokuwepo kwa barabara ya Mchichili - Liyanilo na Nahanga – Chiwime na ubovu wa barabara ya Ruangwa - Mandawa

**4. KATA YA MBWEMKURU**

Kabla ya kutoa taarifa ya kata yake Mh.Diwani wa kata ya Mbwemkuru alitoa taarifa kwamba ule mgogoro wa kugombea makao makuu ya kata sasa umekwisha,hivyo makao makuu ya kata sasa yapo katika kijiji cha Machang'anja na tayari ujenzi wa ofisi ya kata umeanza.

Kwa upande wa changamoto:-ubovu wa barabara ya Ruangwa-Nangurugai ,kutokamilika kwa daraja la Mbwemkuru linalounganisha wilaya ya Ruangwa na Liwale,upungufu wa watumishi wa kada ya Elimu ,Afya kilimo na mifugo na maendeleo ya jamii,aliomba Halmashauri ione uwezekano wa kupeleka watumishi hao,Kukosekana kwa nyumba za watumishi ,tatizo la kuvuja baadhi ya sehemu katika zahanati ya Nangurugai, kutokuwepo kwa huduma ya shule katika kijiji cha Chiundu, Kitongoji cha Mangukwa ambapo jamii ilianzisha ujenzi wa darasa la awali ujenzi ambao haujakamilika hivyo anaomba Halmashauri kuunga mkono nguvu za jamii . Pia Vijiji vya Machang'anja , Chiundu na Chikwale havina Zahanati ,lakini tayari wananchi wameanza kazi ya kufyatua tofali kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati wanaomba nguvu za Halmashauri

**5.KATA YA MAKANJIRO**

Mhe.Kawale alitoa shukrani kwa Halmashauri kwa kuunga mkono nguvu za wananchi katika miradi ya maendeleo.

**6. KATA YA LIKUNJA**

Kwa mujibu wa Mhe.Issa Ngongonda Diwani wa kata hiyo alizungumzia changamoto Katika kata ya Likunja ni wananchi kutokuhudhiria vikao/mikutano ya hadhara ya vijiji.Pia kukosekana kwa ushirikiano baina ya wananchi na Viongozi wao na changamoto nyingine ni baadhi ya wafanyabiashara kukwepa kulipa ushuru.

**7. KATA YA CHIENJERE**

Hakukuwa na changamoto zaidi ya shukrani kutoka kwa diwani wa kata kwa Halmashauri Kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa Zahanati ya Mibure.

**8.KATA YA NANGANGA**

Mhe. Kambona aliwasilisha changamoto za kata ya Nanganga kwa kueleza kuwa zipo changamoto ambazo ni pamoja na:- Kutokuwepo kwa barabara ya kutoka Zahanati ya Mtakuja hii ni baada ya kukosekana kwa kalavati katika barabara ya kwenda Zahanati hiyo, Ameomba Halmashauri kusaidia ukamilishaji wa ujenzi wa ofisi ya kijiji cha Mtakuja ambao umefikia hatua ya rinta. Kata ya Nanganga haina Afisa Maendeleo ya Jamii,Afisa Mifugo pamoja na upungufu wa watumishi wa kada ya Afya na Elimu na ukosefu wa nyumba za watumishi.

**9. KATA YA MALOLO**

Kwa mujibu wa taarifa ya kata ya Malolo ambayo iliwasilishwa na Mh.Mwambe,moja ya Changamoto ni Ukosefu wa nyumba za walimu shule ya msingi Mtawilile,Upungufu wa wataalam,katika kada za kilimo,mifugo,watendaji wa Vijiji na wahudumu wa Afya.Pia ukosefu wa rasilimali fedha unaosababisha kukwamisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kukosekana kwa Ofisi ya Mtendaji wa Kata .

**10. KATA YA NAMICHIGA**

Changamoto zilizopo katika kata hiyo ni pamoja na:- Migogoro ya mipaka kati ya Namichiga na Muhuru.

**11. KATA YA RUANGWA**

Mhe.Pendeka Diwani wa kata ya Ruangwa alieleza kwamba changamoto kubwa kwenye kata yake ni pamoja na kutokuwepo kwa kituo cha Afya ambapo tayari uongozi wa kata umeshatafuta eneo la ujenzi wa kituo cha Afya na kuandaa hamasa kwa wananchi kuanza kufyatua tofali kwa ajili ya ujenzi. Pia kuvamiwa kwa eneo la shule ya sekondari ya Ruangwa.

**12.KATA YA MANDARAWE**

Changamoto ambazo zimewasilishwa katika kata ya Mandarawe ni pamoja na:- Upungufu wa watumishi katika kada zote,Upungufu wa vyumba vya madarasa shule ya msingi Nachinyimba,Upungufu wa vyoo shule ya msingi Mandarawe pia Zahanati ya Nandenje wananchi wameanzisha ujenzi wa nyumba ya mganga wanaomba nguvu za Halmashauri

**13. KATA YA MBEKENYERA**

Taarifa iliwasilishwa na Mh. Zainabu Mnunduma Diwani VIti Maalum changamoto ambazo ziliwasilishwa ni pamoja na Kutokuwepo kwa Mtendaji wa Kata katika kata hiyo,Ubovu wa barabara ya mbekenyera – Mkwana kutokana na ubovu wa kalavati,na kukwama kwa ujenzi wa wodi ya Zahanati ya Mbekenyera baada ya fedha kuisha.

**13.KATA YA LUCHELEGWA**

Kwa mujibu wa Mhe.Diwani wa kata ya Luchelegwa alieleza kuwa changamoto za kata hiyo ni:- Ujenzi wa nyumba ya mwalimu shule ya msingi Nandanga umeanza aliomba nguvu ya Halmashauri, Kata imeanzisha ujenzi wa shule ya sekondari michango inakusanywa hivyo anatarajia kujenga vyumba viwili (2) vya madarasa mpaka kufikia mwezi Januari 2018 wanafunzi wa kidato cha kwanza waanze kusoma.

**15. KATA YA CHIBULA**

Mhe. Songea aliwasilisha taarifa ya kata yake ya Chibula ambayo haikuwa na changamoto zaidi ya zile aliziwasilisha katika robo ya pili ya mwaka 2016/2017.

**16.KATA YA CHUNYU.**

Katika kata ya chunyu changamoto ambazo ziliwasilishwa ni pamoja na ,Kutoanza kazi Zahanati ya Mihewe kwa kuwa bado haijakamilika ,Barabara ya Ruangwa –Mihewe kuna maeneo korofi yenye mawe ameomba yaondolewe, Kutohudhuriwa kwa mikutano ya vijiji.

**17.KATA YA NKOWE**

Mhe.Chitanda Diwani wa kata ya Nkowe aliwasilisha taarifa ikimbatana na changamoto ambazo ni:Ubovu wa barabara ya Mpumbe –kipindimbi pamoja na barabara ya kutoka Mpumbe –Sekondari na KIjiji cha Mpumbe kutokuwa na Mtendaji wa kijiji.

**18. KATA YA CHINONGWE**

Changamoto zilizojitokeza katika kata ya chinongwe ni pamoja na:-

Kukwama kwa ujenzi wa jengo la utawala shule ya sekondari ya Chinognwe,uwepo wa viporo vya ujenzi wa nyumba za walimu na maabara ya shule ya sekondari Chinongwe, upungufu wa vyumba vya madarasa shule ya msingi Juhudi,Kutokuwepo kwa kituo cha Afya kutokuwepo kituo cha afya kjiji cha Litama, Uchakavu wa jengo la Zahanati kijiji cha Likwachu ,Ukosefu wa barabara ya Litamba –Mbaju na Ukosefu wa miundombinu ya kusambaza maji kutoka Chinongwe A-kwenda Juhudi A na B na Chinongwe- Litama

**19. KATA YA NANDAGALA**

Kwa mujibu wa taarifa kutoka katika kata ya Nandagala imeeleza kuwa kata inakabiliwa na changamoto ambazo ni:-Uhaba wa nyumba za walimu,Uhaba wa vyumba vya madarasa, Wananchi kutoshiriki katika kazi za ujenzi wa Taifa

**20.KATA YA NAMIBILANJE**

Taarifa ya kata ya Nambilanje iliwasilishwa na Mh.Chigope ambaye ni diwani wa kata ya Nambilanje katika taarifa hiyo hakukuwa na changamoto.

**MJADALA**

Kaimu Mkurugenzi ambaye alikuwa katibu wa kikao alimuomba Mh.Mwenyekiti kuwaruhusu baadhi ya wakuu wa idara kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja/changamoto za wajumbe.

Mkuu wa idara ya afya alieleza kuwa anatambua changamoto za zahanati ya Nangurugai,ameshauri waangalie fedha za uchangiaji na zile za tumaini la Mama ili kuona namna ya kufanya ukarabati.

Mhe. Chande yeye alizungumzia kuhusu ushuru wa zao la mbaazi kukusanywa na Halmashauri badala ya vijiji alisema kuwa utaratibu huu unachelewesha upelekaji wa wa fedha vijijini Pia alizungumzia kuhusu

mkanganyiko wa takwimu za ushuru wa mbaazi kutoka vijijini hadi Halmashauri, alieleza kuwa kwa kiasi fulani watendaji wa kata na vijiji wamehusika kwa kushirikiana na wafanyabiashara ifike wakati wabainike ili hatua zichukuliwe.

Mhe.Mwenyekiti alieleza kuhusu ushuru wa mbaazi kukusanywa na Halmashauri ni kutokana na baadhi ya watendaji kutokuwa waaminifu kwani baadhi yao walikuwa hawafikishi fedha benki,lakini kwa kukusanywa na Halmashauri fedha zinaingizwa kwenye akaunti za vijiji.

Mkuu wa Idara ya Fedha alitoa ufafanuzi kwa kusema kwamba changamoto kubwa baadhi ya vijiji havina akaunti namba au akaunti zao zimelala jitihada zimefanyika za kuwakumbusha Watendaji wa Vijiji ambao akaunti zao zimelala au kufungwa ili kuzifufua lakini muitikio wake ni mdogo sana,

Mkuu wa idara ya ujenzi alizungumzia kuhusu ujenzi wa barabara ya Ruangwa –Nangurugai kwamba tayari Mzabuni alishapatikana na kazi itaanza hivi karibuni.

Kuhusu ujenzi wa daraja la Mbwemkuru alieleza kuwa tayari fedha Tshs. 900,000,000/- imetumwa kwa Halmashauri ya Ruangwa na Liwale na tarehe 28/5/2017 Wahandisi wa Wilaya ya Ruangwa na Liwale pamoja na wataalamu kutoka ofisi ya mkuu wa Mkoa watakutana kwa ajili ya kufanyakazi ya usanifu wa daraja hilo ili ifikapo mwezi Septemba 2017 kazi ya ujenzi ianze.

Kuhusu barabara za Nahanga –Chiwime na Mchichili –Liyamilo bado hazipo kwenye mpango wa Halmashauri ila alitoa ushauri kwa jamii kuanza kuzitengeneza kienyeji kwa kutumia nguvu zao.

Mhe.Omari Songea alishauri kuhusu wananchi wanaochimba madini maeneo ya barabara kutoka kijiji cha Mkaranga ni vyema sheria ichukue mkondo wake haswa suala la uchimbaji wa madini katika maeneo ya barabara ili kudhibiti hifadhi ya mazingira.

Mhe.Mwenyekiti pia alizungumzia suala la ujenzi wa vituo vya polisi kama baadhi ya wajumbe walivyoomba amesema kuwa suala hilo ni la kijamii zaidi wala sio kusubiri Serikali kikubwa jamii yenyewe ijenga kituo na Serikali italeta askari.

Kaimu MKurugenzi alihitimisha kwa kueleza kuwa changamoto za wajumbe zimechukuliwa na ofisi kwa ajili ya kuzifanyia kazi .

Baada ya majadilianao hayo wajumbe walitoa maazimio yafuatayo:-

- Sheria ya hifadhi ya barabara zitumike kuwaondoa watu wanaochimba madini katika eneo la barabara ya Namichiga-Nambilanje katika kijiji cha Mkaranga ,pamoja na maeneo mengine ambayo uchimbaji wa madini unafanyika katika hifadhi ya barabara.

- Ofisi ya Mkurugenzi iwabaini waliohusika katika udanganyifu uliojitokeza katika ununuzi wa zao la mbaazi 2016 na kusababisha mkanganyiko wa takwimu na wakishabainika wachukuliwe hatua.

- Kuhusu 20% inayorejeshwa vijijini kutokana na mapato ya ndani lirudi katika kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango ili kuona namna bora ya kurejesha 20% ya vijiji.

•

**AGENDA NA. 3/5/2017 MASWALI NA MAJIBU**

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa amepokea majina ya Madiwani 8 ambao wameomba kuuliza maswali mbele ya kikao cha baraza.

Mhe. Liwikila Diwani wa kata ya Matambalare aliulizia idadi ya watumishi hewa waliobainika katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa na sekta ipi imeathirika zaidi.

Mhe.Mwenyekiti alijibu kwa kueleza kwamba Halmashauri haina watumishi hewa,isipokuwa kuna baadhi ya watumishi wamebainika kutumia vyeti bandia na idara iliyoathirika sana ni idara ya afya.

Mhe.Omari Songea alitaka kujua lini Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa watalipwa posho ya mwezi Novemba 2015 mara baada ya uchaguzi Mkuu.

Mhe.Mwenyekiti alijbu kwa kueleza kuwa jambo hili lilizungumzwa katika kikao cha ALAT taifa lakini hadi sasa Serikali haijatoa tamko. Pia Afisa Utumishi alieleza kuwa hoja hii ilishajibiwa katika vikao vya Baraza la Halmashauri .

Pamoja na majibu hayo wajumbe hawakuridhika ndipo walitoa agizo.

**AGIZO:**Mkurugenzi Mtendaji afanye mawasiliano na ofisi ya mkuu wa mkoa ili kuweza kutoa mwongozo kuhusu malipo ya posho ya mwezi Novemba 2015

Mhe.Mpanyangula aliuliza kwamba kwa kuwa 20% ya fedha za vijiji hazilipwi,nini hatima ya posho za wenyeviti wa vijiji.

Majibu yalitolewa kuwa Halmashauri ilishaamua kuwa posho za wenyeviti wa vijiji zilipwe kwa kutumia mapato ya vijiji.

Mh.Kitatichingi aliuliza kuhusu kijiji cha Namkatila ambacho kimeanzisha ujenzi wa Zahanati ni lini Halmashauri itaunga mkono wananchi hao,ikiwa jengo limefikia hatua ya rinta.

Majibu yalitolewa kuwa Halmashauri imejiwekea utaratibu wa kusaidia miradi ya maendeleo na kutekelezwa na wananchi kwa kutumia mapato ya ndani, changamoto iliyoko ni upatikanaji wa fedha,pindi fedha ikishapatikana Halmashauri itaunga mkono katika hatua ya kupauiliwa kwa jengo hilo.

Mhe.Chigope aliuliza kuhusu vijiji kutopewa fedha za maendeleo zilizotokana na makato ya zao la korosho.

Mhe. Mwenyekiti alijibu kwa kueleza kuwa katika misimu miwili (2) iliyopita fedha za maendeleo hazikukatwa kwa mujibu wa mwongozo wa Bodi ya korosho.Hata hivyo katika kikao cha wadau wa korosho jambo hilo la kuchangia mifuko ya maendeleo lilizungumzwa na kwamba Bodi ya korosho imelipokea kwa ajili ya kulifanyia kazi.Pia Halmashauri zitapewa maelekezo ya nini cha kufanya kuhusu fedha za maendeleo.

**AGENDA NA. 4/5/2017 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE**

**1-2/2/2017**

Kwa kuwa muhtasari ulifika kwa wajumbe siku saba kabla ya kikao,muhtasari ulihesabika kuwa umeshasomwa,hivyo wajumbe walifanya marekebisho kadhaa kabla ya kuthibitishwa .

**MAREKEBISHO**

Uk.wa 1 katika majina ya wajumbe wasiohudhuria liongezwe jina la Daniel Mtawa ambaye ni mgonjwa.

Baada ya marekebisho hayo wajumbe walithibitisha muhtasari kwa kuwekwa saini za mwenyekiti na katibu ili kuwa kumbukumbu sahihi ya Halmashauri.

**AGENDA NA.5/5/2017 KUPITIA NA KUJADILI MIHITASARI YA KAMATI ZA KUDUMU**

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa wenyeviti wa kamati za kudumu wanatakiwa kuwasilisha mihtasari ya kamati za kudumu kwa vikao vilivyofanyika katika robo ya tatu ya mwaka 2016/2017.

**1.KAMATI YA FEDHA,UONGOZI NA MIPANGO**

Mhe.Makamu mwenyekiti wa Halmashauri kwa niaba ya mwenyekiti wa Halmashauri ambaye ndie mwenyekiti wa kamati hii aliwasilisha mihtasari mitatu ya vikao vya:-

- Tarahe 24/1/2017
- Tarehe 21/2/2017
- Tarehe 23/3/2017

Baada ya kuwasilisha wajumbe walianza mjadala wa mihtasari hiyo .

Mhe.Omari Pendeke alitaka kujua nini hatima ya fedha Tshs. 591,635,334 za malipo ya korosho katika msimu wa mwaka 2016/2017 ambazo wakulima wanazidai kutoka vyama vya ushirika vya msingi na lini wakulima hao watalipwa fedha hizo.

Majibu yalitolewa na makamu mwenyekiti kuwa wakulima waliokuwa wanadai fedha hizo ilitokana na baadhi ya watendaji wa vyama vya msingi kutokuwa na taaluma ya ushirika na kushindwa kukokotoa hesabu,hata hivyo kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa katika kikao cha wadau wa korosho MKoa ulieleza kuwa hakuna mkulima ambae anadai malipo ya Korosho.

Mhe.Chikongwe Diwani wa kata ya Nandagala alitaka kufahamu ni lini fedha za umwagiliaji Nanganga utekelazaji wake utaanza kwani mpaka sasa hakuna kinachofanyika.

Makamu mwenyekiti alijibu kwa kueleza kuwa fedha hizo zimekuja lakini hazitoshi kufanya utekelezaji,hivyo ofisi ya Mkurugenzi iliwaita wataalamu wa umwagiliaji kanda ili kuja kufanya tathimini /upembuzi yakinifu ili kujua gharama halisi za mradi ili waweze kuishauri Halmashauri na kutoa tamko nini cha kufanya.

Maelezo ya nyongeza yaliyotolewa na mkuu wa idara ya kilimo kwamba kazi ya tathimini ilikuwa inagharimu fedha TShs.100,000,000/- ambazo Halmashauri haina fedha hizo ndipo iliamua kuwaita watu wa umwagiliaji kanda ili waje watoe maelezo na kuieleza Wizarani sababu za kukwama kwa mradi huo.

Kwa upande wake Mh. Mwenyekiti alieleza kuwa watu wa umwagiliaji wamekuja kwa ajili ya kufanya tathimini ni vyema wakamilishe kazi hiyo na kutoa ripoti Wizarani ili zabuni ya mradi itangazwe na kazi ianze kufanyika.

Mhe. Pendeka yeye alizungumzia kuhusu kutokamilka kwa mradi wa maji Mbekenyera aliomba ufafanuzi nini kimekwamisha.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa kinachocheleweshа ni suala la kuingiza umeme kwenye pampu za maji.

Kwani awali mpango ulikuwa kufunga Jenereta na kuwa kuingiza umeme wa REA ni imani ya Halmashauri kuwa mpaka mwisho wa robo ijayo ya mradi utakuwa umekamilika.

Mhe.Songea alihoji kuhusu fedha TShs. 55,000,0000/= za kukamilisha ujenzi wa shule ya sekondari ya Kasimu Majaliwa ikiwa wadau walichangia fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo.

Mkuu wa idara ya mipango alitoa ufafanuzi kwamba bajeti ya ujenzi wa shule hiyo ni TShs.131,000,000/= awamu ya kwanza ilitolewa idhini ya kutumia TShs.75,000,000/=,kati ya hizo fedha kiasi 19,000,000/=. kilitolewa kwa ajili ya kulipa fidia ya maeneo ya watu ambayo yamechukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo.

Mpango ulikuwa Halmashauri kujenga madarasa 3 kata ya Ruangwa na kata ya Nachingwea kujenga madarasa 3 hata hivyo wananchi walichangia TShs.3,000,000/=tu .

Kutokana na hali hiyo fedha kwa ajili ya ujenzi TShs.75,000,000/= hazikuweza kutosha ndipo Halmashauri iliomba fedha za nyongeza TShs.55,000,000/= kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo.Kuhusu wadau waliochangia baadhi yao hawajalipa fedha hizo,hata hivyo ofisi imewaandikia barua za kuwakumbusha.

Baada ya mijadala hiyo hatimaye wajumbe waliipitisha mihatasari ya kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango.

**2. KAMATI YA ELIMU AFYA NA MAJI**

Mhe.mwenyekiti wa kamati ya Elimu,Afya na Maji Mh.Eliasi Nkane aliwasilisha muhtasari wa kikao cha tarehe 17/01/2017.

**MAJADILIANO**

Wajumbe walitaka kujua mwendelezo wa taarifa ya kamati ndogo ya Elimu,Afya na Maji kwa ajili ya kutafuta suluhu ya mgogoro wa shule ya sekondari ya Ruangwa.

Katika kujibu hoja hiyo mwenyekiti wa kamati alieleza kuwa baada ya kamati kumaliza kazi yake iliwasilisha taarifa mbele ya kamati ya Elimu,Afya na Maji ikiwa na mapendekezo yake.Hata hivyo Mkurugenzi alishauri

kwa kusema kuwa Mkuu wa Mkoa alifika shuleni Ruangwa sekondari na kuunda kamati nyingine kutokana na hali hiyo alishauri kwamba tusubiri kamati ya mkuu wa Mkoa, ili kupata utekelezaji wa pamoja.

Pia Mhe.Mwenyekiti wa Halmashauri alieleza kuwa kuna baadhi ya mabadiliko katika shule hiyo yamefanyika katika kupunguza mgogoro,hata hivyo mwenyekiti alitoa ahadi ya kutolewa taarifa ya utekelezaji kuhusu mgogoro huo kupitia kamati husika.

Mhe.Zainabu Mnunduma alitaka kujua ni hatua zipi zinachukuliwa kwa mwanafunzi ambaye anaacha shule kwa makusudi kwani kuna kundi kubwa la wanafunzi wa sekondari ambao wanaacha shule bila sababu za msingi.

Ufafanuzi ulitolewa na mwenyekiti wa kamati kwa kusema kuwa kuwa zipo sheria za mahudhurio ya lazima kwa wanafunzi ambazo zinatakiwa na kusimamiwa kuanzia ngazi ya Familia hadi Taifa, kinachotakiwakama mtoto ameacha shule mzazi anapaswa kutoa taarifa kwa uongozi wa kijiji au kata ili aweze kuchukuliwa hatua.

**AZIMIO:**Wajumbe walipitisha muhtasari wa kamati ya Elimu,Afya na Maji.

**3.KAMATI YA UCHUMI,UJENZI NA MAZINGIRA**

Mhe.Rashidi Mnunduma mwenyekiti wa kamati ya Uchumi,Ujenzi na Mazingira aliwasilisha muhtasari wa kikao cha tarehe 19/1/2017.

**MAJADILIANO**

Mhe.Mbute alitoa hoja kuhusu suala la fedha za michango ya pembejeo za korosho ambazo zimekusanywa na vyama vya msingi kufuatia agizo la Serikali kwamba pembejeo za korosho zitaletwa na zitagawiwa kwa wakulima bure,Je fedha hizo zitarejeshwa kwa wakulima?

Mhe.mwenyekiti wa kamati alitoa majibu kwamba ni vyema fedha ziendelee kukusanywa kwa kuwa haijajulikana kama pembejeo za ruzuku zinaweza kutosha,hivyo basi kwa kukusanya fedha kutoka kwa wakulima itasaidia kununua pembejeo za ziada kwa ajili ya kufidai upungufu kwani salfa iliyoagizwa ni tani 18 tu.

Mhe.Likuche alieleza kuwa ipo kampuni ya Ngwena ambayo inafanya uthamini wa mali za wananchi katika maeneo ambayo shughuli za uchimabji wa madini utafanyika katika kijiji cha Nangurugai lakini mpaka sasa hakuna malipo yoyote yaliyofanyika na kampuni hiyo kwa wananchi kwenye maeneo hayo.

Mwanasheria wa Halmashauri alitoa ufafanuzi kwamba uthamini wa mali ukifanyika na kufika miezi sita bila kufanya malipo,uthamini unafanyika tena,hata hivyo Kampuni hiyo imesema haifanyi uthamini mpaka ipate leseni na hilo ni jambo la kisheria.

**AGIZO:-** Ofisi ya Mkurugenzi ifanye mawasilano na ofisi ya mkuu wa Wilaya ili kujua nini kinaendelea kuhusu Kampuni ya Ngwena inayofanya utafiti wa madini katika kijiji cha Nangurugai.

Mhe.Chembe alieleza kuhusu ujenzi wa barabara ya Ipingo-Chinongwe na Nandanga –Luchelegwa ambayo awali ilifanyiwa matengenezo wakati wa ujio wa mke wa Mhe.Waziri Mkuu lakini cha kushangaza barabara hiyo imefanyiwa matengenezo mengine ya kuchongwa.

Mkuu wa idara ya ujenzi alitoa ufafanuzi kuwa barabara hiyo ipo kwenye bajeti ya matengenezo ya mwaka 2016/2017 hivyo fedha za mfuko haziwezi kutumika nje ya sheria,sera ya maelekezo ya mfuko wa barabara kama inapangwa kufanyiwa matengenezo ni lazima yafanyike. Aliongeza kwa kusema kuwa TANROAD ilichonga barabara ya Luchelegwa-Nandanga ambayo haikuwa ndani ya bajeti.Pia Halmashauri ilitenga fedha kwa ajili ya matengenezo madogo yaani kuchonga kwepesi na ndio kazi iliyofanyika isingewezekana fedha za barabara hiyo zikatumike kutengeneza barabara nyingine na kwamba mhandisi yupo tayari kuwasilisha nyaraka zote kuhusu matengenezo ya barabara hiyo kama mjumbe atahitaji.

**AZIMIO:**Wajumbe walipitisha muhtasari wa kamati ya Uchumi,Ujenzi na Mazingira wa tarehe 19/1/2017.

**4.KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI**

Makamu mwenyekiti ambaye mwenyekiti wa kamati hii aliwasilisha muhtasari wa tarehe 5/1/2017.

**AZIMIO:** Wajumbe walipitisha muhtasari wa kikao cha kudhitibi Ukimwi cha tarehe 5/1/2017.

**AGENDA NA.6/5/2017 TAARIFA YA MKURUGENZI**

Mkurugenzi aliwasilisha taarifa mbele ya kikao iliyoeleza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa katika kipindi cha Januari 2017 hadi sasa inaendelea na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo. Shughuli zilizotekelezwa kisekta ni kama ifuatavyo;

**1. Sekta ya Elimu**

Ufanyikaji wa Mitihani darasa la Nne na la saba,Ujenzi wa Miundombinu ya Shule Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kupitia mradi wa **P4R** ilipata kiasi cha Tsh. 132, 000, 0000/= kwaajili ya ujenzi wa vyumba sita vya madarasa, ukarabati wa madarasa mawili na ujenzi wa matundu 20 ya vyoo katika shule ya msingi Mbekenyera

Vilevile Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa imendelea kuunga mkono nguvu za wananchi kwa kuchangia fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika sekta za afya na elimu, Uchangiaji huu umegharimu **TSH 98,885,000/=**

**Elimu Sekondari**

**Ufanyikaji wa Mitihani Kidato cha Pili**

Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa imeratibu ufanyikaji wa mitihani ya kidato cha pili mwaka 2016 ambayo ilifanyika Novemba, 2016 Jumla ya watahiniwa 676 walifaulu mitihani yao hivyo Halmashauri imeshika nafasi ya 2 katika Mkoa wa Lindi. Ufanyikaji wa Mitihani Kidato cha Nne ambayo ilifanyika Oktoba, 2016 Wataalamu wanaendelea na uchambuzi ili kuleta taarifa ya ufaulu wa mtihani huo. **Miundombinu ya Shule** Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kupitia mradi wa **P4R** ilipata kiasi cha Tsh. 132, 000, 0000/= kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vitano vya madarasa, ukarabati wa ofisi, jiko na ujenzi wa matundu 20 ya vyoo katika shule ya Sekondari Mbekanyera.

Mradi huu umekamilika kwa asilimia mia. Aidha baada ya miradi ya P4R kuonekana imefanya vizuri wafadhili wamepanua ufadhili na kutoa fedha Tsh 156,000,500/= ambapo Tsh. 95,000,500/= zimepelekwa Mnacho Sekondari na 61,000,000/= zimepelekwa Namichiga Sekondari. Wakati wowote miradi itaanza.Halmashauri ilichangia Tsh 75,000,000/= kwaajili ya ujenzi wa madarasa matano, vyoo matundu 9. Mh. Mbunge kupitia mfuko wa Jimbo amechangia Tsh 33,000,000/= katika ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Kata ya Nachingwea.

**Ukusanyaji wa mapato.**
Halmashauri inaendelea na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kupitia vyanzo vya ndani ambapo katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2016 jumla ya shilingi 662,596,953/= sawa na asilimia 17% ya makisio ya mwaka na asilimia 71.28 ya lengo la robo mwaka la Tshs 929,665,400/=.

**Matengenezo ya barabara za wilaya.**
Halmashauri imetoa kazi kwa wazabuni kufanya matengenezo ya barabara ya kawaida, sehemu korofi, muda maalum, ujenzi wa makalavati na madaraja katika barabara za wilaya zenye urefu wa km. 179.65. Pia Km 3.95 zimeanza kujengwa kwa kiwango cha lami katika maeneo ya mji wa Ruangwa.

**Maandalizi ya Kilimo kwa Msimu wa 2016/2017.**
Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2016/2017, Wilaya imelenga kulima hekta 86,179 za mazao ya chakula wanga na protini (mahidi, mhogo, mtama, mpunga nk ) mavuno yanayotarajiwa ni tani 147,005. Pia Hekta 35,903 za mazao ya biashara na **Upandaji wa Mikorosho Mipya 5,000 kwa kila Kijiji** ,

Kwa upande wa **ununuzi wa korosho msimu 2016/2017.**

Zoezi la ukusanyaji na uuzaji wa zao la korosho unaendelea ambapo hadi tarehe 16/01/2017 jumla ya tani 10,137.735 zilikuwa zimekusanywa katika maghala ya vyama vya msingi. Jumla ya tani 10,117,907 zilikuwa zimeshasafirishwa kwenda ghala kuu Nachingwea na tani 10,082,216 zilikuwa zimeshauzwa katika minada kumi na mbili iliyofanyika Nachingwea, Liwale na Ruangwa kwa tarehe tofauti tofauti.

**SEKTA YA AFYA**

Kwa ujumla upatikanaji wa dawa muhimu za binadamu katika Hospital ya Wilaya, Vituo vya afya na zahanati zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa iko kama ifuatavyo kwa wastani;

| Hospitali ya Wilaya | Vituo vya Afya | Zahanati |
|---|---|---|
| 90% | 80% | 80% |

**1. Miundombinu ya Afya:**
Ujenzi wa Hospital ya Wilaya, wodi za kituo cha afya cha Mbekenyera na zahanati za vijiji vya Mibure, Mkutingome na Namilema uko katika hatua mbalimbali pia **Ufunguzi wa Zahanati mpya** ambapo Zahanati tano zimeanza kufanya kazi .

**SEKTA YA ARDHI NA MALIASILI**

Idara imeendelea kufanya utatuzi wa Migogoro ya Mipaka kati ya Vijiji na Vijiji na Wilaya na Wilaya.

**SEKTA YA MAJI**

**2. Uchimbaji wa visima vya maji vijijini.**
Baada ya kazi ya utafiti wa maji chini ya ardhi kwa ajili ya kutambua sehemu zifaazo kwa ajili ya uchimbaji wa visima kukamilika kupitia katika vijiji 8 Kazi inayoendelea hivi sasa ni usanifu (topographic survey) ili kujua gharama za mradi katika vijiji tajwa kazi ambayo itakamilika Februari, 2017.

Kwa upande wa Utawala Halmashauri ilifanya uratibu wa Ziara ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa, ambae alifanya ziara katika wilaya ya Ruangwa kuanzia tarehe 27-30/12/2016.

Katika ziara hii, Waziri Mkuu alitoa maagizo mbalimbali ambayo Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi wanatakiwa kuyatekeleza.

Halmashauri inaendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyoidhinishwa kwenye Mpango na bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2016/2017.

Pamoja na taarifa hizo pia iliwasilishwa barua yenye maelekezo kuhusu utoaji na usimamizi wa mikataba na zabuni kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa.Kikubwa ambacho kimeelekezwa ni athari za kuendelea kupewa kandarasi/zabuni kwa watendaji wa Halmashauri na madiwani,wenyeviti na Mameya katika Halmashauri wanazoziongoza.Athari ambazo zinapatikana ni pamoja na:-

i. Kutolewa kandarasi/Zabuni kwa upendeleo na kufanya waombaji wengine kukosa.
ii. Kazi zinazofanyika au huduma zinazotolewa zinakuwa chini na kusababisha kukosekana kwa thamani halisi ya kazi au huduma iliyotolewa.
iii. Kuwepo kwa mgongano wa kimaslahi na hatimaye kukiukwa kwa matakwa ya kisheria ya ununuzi wa umma na kanuni zake.

Barua hiyo imepiga marufuku kwa watendaji na madiwani kujihusisha na masuala ya kizabuni/kandarasi katika Halmashauri wanazoziongoza.

**AZIMIO.**

Wajumbe walipokea maelekezo hayo kwa ajili ya utekelezaji.

**AGENDA NA 7/5/2017 KUTHIBITISHA MAAZIMIO**

Jumla ya maazimio 5 yalipitishwa na wajumbe ambayo ni :

i. Sheria ya hifadhi ya Barabara zitumike kuwaondoa watu wanaochimba madini katika eneo la barabara ya Namichiga –Nambilanje katika eneo la Mkaranga pamoja na maeneo mengine ambayo uchimbaji wa madini unafanyika katika hifadhi ya Barabara.

ii. Ofisi ya Mkurugenzi iwabaini watu waliohusika na udanganyifu uliojitokeza katika ununuzi wa zao la mbaazi 2016 na kusababisha kutokea mkanganyiko wa takwimu na wakishabainika wachukuliwe hatua.

iii. Mkurugenzi afanye mawasiliano na mkuu wa Wilaya ili kuja nini kinaendelea kwa kampuni ya madini ya Ngwena inayofanya tahtmini katika kijiji cha Nangurugai

iv. Mkurugenzi Mtendaji afanye mawasiliano na ofisi ya Mkuu ya Mkoa ili kupata mwongozo kuhusu malipo ya posho ya madiwani ya mwezi Novemba 2015.

**AGENDA NA.8/5/2017 KUFUNGA KIKAO**

Mhe.Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 10.30 jioni kwa kuwashukuru wajumbe kwa michango yao pia amewasisistiza waheshimiwa wajumbe kwenda kuyafanyia kazi yale yote yaliyojadiliwa katika kikao hiki na kuyafikisha kwa wananchi kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wilaya,pia aliwataka watendaji wa Halmashauri kuendelea kufanya kazi kwa bidii.

**UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| …………………………. | ....…………………….. |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

……………..

**TAREHE**